# Orodha ya stadi: Vifaa saidizi vya kutembea

TAP

| Mwanafunzi: | Mwezeshaji: | Tarehe: |
|---|---|---|

| Sifa | Maelezo ya Mwezeshaji | Ndio | Hapana |
|---|---|---|---|
| **Hatua ya kwanza: Chagua** | | | |
| 1. Kusanya taarifa sahihi kwa kutumia fomu ya tathmini: chauga kifaa saidizi cha kutembelea ambacho kinakidhi mahitaji ya mgonjwa. | | | |
| 2. Inaainisha pale ambapo mtu anapohitaji rufaa na kwenda kwenye huduma sahihi. | | | |
| **Hatua ya pili: Kipimo sahihi** | | | |
| 3. Mpe mtu kifaa saidizi sahihi cha kutembelea:<br>• Kinamfanya mtu kuweza kuwa katika mkao mzuri<br>• Weka kifaa saidizi cha kutembelea katika kipimo sahihi<br>• Angalia kama ni kipimo sahihi kwake | | | |
| **Hatua ya tatu: Fundisha** | | | |
| 4. Mfundishe mtu namna ya kutumia kifaa saidizi cha kutembelea ( katika mazingira husika)<br>• Kuanzia kukaa hadi kusimama<br>• Kutembea<br>• Kupanda na kushuka ngazi | | | |
| 5. Mfundishe mtu namna ya kutunza kifaa saidizi cha kutembelea:<br>• Dondoo za kukikagua na kubadilisha vitu vilivyoharibika.<br>• Utunzaji wa jumla wa kifaa | | | |
| 6. Taarifa za ufuatiliaji wa kifaa saidizi kwa mtumiaji.<br>• Pale ufuatiliaji unapotakiwa<br>• Dalili za tahadhali za kiafya (angalia sehemu ya kukanyagia ya miguu kila siku, na hatari ya kuanguka. | | | |
| **Hatua ya nne: Ufuatiliaji** | | | |
| 7. Fuatilia mambo sahihi ya ufuatiliaji kwa kulingana na tathmini iliyofanyika kwa mara ya pili kama vile:<br>• Kuchagua kifaa saidizi cha kutembelea kingine.<br>• Kurekebisha kifaa saidizi cha kutembelea unachokitumia sasa<br>• Kutoa mafunzo zaidi<br>• Kubadilisha au kurekebisha kifaa cha kutembelea. | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • Toa rufaa kwend kwenye huduma nyingine | | | |
| 8. Fanya marekebisho muafaka:<br>• Kaza nati<br>• Rudishia sehemu za axilla na sehemu za kushikia ambazo zimeharibika<br>• Rekebisha breki za rolata. | | | |
| **Katika hatua zote** | | | |
| 9. Katika hatua zote ;onyesha kuwa kazi yako ni salama na inamlenga mteja | | | |

## Mambo ya kuzingatiwa na Mwezeshaji

**Tumia Orodha hii ya Stadi kukusaidia:**

- Tathmini namna Washiriki wa Mafunzo wanavyotekeleza stadi za za kugawa kifaa saidizi cha kutembelea na kama:
  - Wanaweza kugawa kifaa saidizi cha kutembelea bila kupewa msaada kutoka kwa mtu mwingine, au
  - Wanahitaji mafunzo zaidi ya vitendo na kama ndicho hicho wanachokihitaji, tambua aina ya stadi wanazohitaji kufanyia mazoezi.

**Kumbuka kuwa:**

- Hii Orodha ina Stadi muhimu ambazo ziko kwenye moduli ya TAP.
- Kuna stadi nyingine ambazo ungependa Watoa huduma wako kuwa nazo kulingana na mahitaji ya huduma wanazozitoa. Unaweza kuongeza mambo mengine kwenye Orodha hii kama kwa kufanya hivyo itasaidia zaidi.
- Inawezekana usiweze kuona stadi katika zote katika hatua zote nne katika kipindi kimoja, ukiendelea kufuatilia zitachomoza kwenye tarehe za mbele.

**Ili kutumia Orodha ya Stadi:**

- Fuatilia kwa karibu namna ambavyo Washiriki wa Mafunzo wanagawa vifaa saidizi vya kutembea. Hii naweza kufanyika kwa kufanya igizo (mmoja akiwa Mteja mwingine kama Mtoa huduma) au kufanya igizo na Wateja.
- Kila mara hakikisha kuwa mazoezi na wateja yanafanyika kwa usalama.
- Andika kwenye fomu kama Mshiriki wa Mafunzo amefanya kila stadi kwa usahihi. Andika maelezo kwenye eneo la kutoa maoni. Hii inaweza kuwa vitu ambavyo Mshiriki wa Mafunzo amefanya vizuri zaidi au maeneo ambayo anapaswa kuboreshwa zaidi/anahitaji mafunzo zaidi

**Utoaji wa mrejesho kwa Washiriki wa Mafunzo**

- Jadili na Washiriki wa Mafunzo kuhusu mambo uliyoyaona. Wajulishe mambo wanayoyafanya vizuri na maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa.
- Wape nakala ya Orodha ya Stadi iliyokamilika kwa ajili ya wao kuweka kumbukumbu.
- Endelea kutoa mafunzo kwa vitendo na msaada pale unapohitajika na fanya tathmini mara nyingine ili kuboresha stadi zao na kujenga hali ya kujiamini.

**Ni wakati gani Mshiriki wa Mafunzo anaweza kugawa vifaa saidizi vya kutemelea bila ya kupata usaidizi?**

- Ili kuafnya kipimo cha Uoni kwa usalama zaidi,mshiriki wa mafunzo anapaswa kukamilisha stadi zote kwa usahihi.
- Kumbuka- kutoa mafunzo kwa vitendo na kusimamia ni mchakato endelevu ili kuboresha stadi.